TANGAZO LA SERIKALI Na. 108 la tarehe 14/2/2025

SHERIA YA USIMAMIZI NA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA GARI MOJA LINALOINGIZWA NCHINI NA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA AJILI YA MRADI WA KUTATUA MIGONGANO BAINA YA WANYAMAPORI NA BINADAMU YA MWAKA 2025

Jina na kuanza kutumika

**1.** Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Gari Moja Linaloingizwa Nchini na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa ajili ya Mradi wa Kutatua Migongano baina ya Wanyamapori na Binadamu ya Mwaka 2025, na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 19 Desemba, 2024.

Msamaha

**2.** Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote yanayoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kiasi chote cha ushuru wa bidhaa kinachotakiwa kulipwa kuhusiana na gari moja lililoainishwa kwenye Jedwali, linaloingizwa au kununuliwa ndani ya nchi, kabla ya kibali cha forodha na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mradi wa kutatua mgongano baina ya wanyamapori na binadamu umesamehewa.

Masharti

**3.** Msamaha wa kodi unaotolewa chini ya Amri hii utafika ukomo na ushuru utadaiwa na utatakiwa kulipwa kana kwamba msamaha chini ya Amri hii haukutolewa, iwapo gari husika litatumika kwa matumizi tofauti au litahamishwa, kuuzwa au kwa namna yoyote atapewa mtu mwingine asiyestahili kufaidika na faida zinazotolewa chini ya Amri hii.

Kuisha kwa muda

**4.** Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafika ukomo tarehe 18, Aprili, 2025.

JEDWALI

*(Imetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| SN | Maelezo | Mwaka | Idadi | Namba ya Chassis | Mahali |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Hilux Double Cabin 2.4 TD, RHD | 2024 | 01 | AHTDB8CD705636364 | limeingizwa |

Dodoma,
……………..., 2025

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*